



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA
KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA
UBUNGE KATIKA JIMBO LA TEMEKE NA UDIWANI KATIKA
KATA 46 ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Temeke katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke Mkoani Dar es Salaam baada ya aliyekuwa mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa **Maulid Said Abdallah Mtolea** kujiuzulu uanachama wa Chama cha Wananchi (CUF).

Vile vile Tume imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata 46 za Tanzania Bara. Nafasi hizo wazi zimetokana na vifo, kujiuzulu na kuvuliwa uanachama kwa baadhi ya Madiwani.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 37 (1) (b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, pamoja na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuhusu uwepo wa Uchaguzi mdogo wa Ubunge

katika Jimbo la Temeke na wa Udiwani katika Kata Arobaini na Sita (46) zilizopo katika Mikoa Kumi na Nne (14) na Halmashauri Ishirini na Nane (28) za Tanzania Bara.

Tume imepanga kuendesha Uchaguzi huo Mdogo wa Ubunge Jimbo la Temeke na Udiwani katika Kata hizo 46 kwa kuzingatia Ratiba ifuatayo:

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 14 hadi tarehe 20, Desemba mwaka huu.
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 20, Desemba mwaka huu
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 21, Desemba mwaka huu hadi tarehe 18 Januari 2019 na
4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 19 Januari 2019

Tume inapenda kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi huu mdogo.

Imetolewa leo tarehe 06 Desemba, 2018.

Jaji (R) Semistocles S. Kaijage

MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

KATA ZILIZOWAZI

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
1.	ARUSHA	1.	Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro	1	Sale
				2	Misigyo
				3	Malambo
				4	Orgosorok
				5	Olorien/Magaiduru
		2.	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	6	Kimnyak
2.	LINDI	3.	Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa	7	Kiranjeraje
				8	Kikole
				9	Pande Mikona
		4.	Halmashauri ya Wilaya ya Liwale	10	Kichonda
				11	Mlembwe
3.	MANYARA	5.	Halmashauri ya Wilaya ya Babati	12	Dareda
				13	Magara
		6.	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	14	Makame
		7.	Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro	15	Loiborsiret
				16	Ruvu Remit
				17	Naberera

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
4.	MWANZA	8.	Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba	18	Walla
		9.	Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema	19	Nyampulukano
5.	MOROGORO	10.	Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga	20	Msogezi
		11.	Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero	21	Mtibwa
				22	Tchenzema
				23	Mangae
12.	Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa	24	Magomeni		
6.	DARES SALAAM	13.	Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	25	Keko
		14.	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	26	Magomeni
7.	KIGOMA	15.	Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu	27	Kitanga
		16.	Halmashauri ya Mji wa Kasulu	28	Kigondo
				29	Msambara
17.	Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe	30	Mnyegera		
8	KAGERA	18.	Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba	31	Buhendangabo

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
				32	Nyakato
				33	Kikomelo
		19	Halmashauriya Wilaya ya Misenyi	34	Kanyigo
		20	Halmashauri ya Wilaya ya Ngara	35	Nyamiaga
9.	RUVUMA	21	Halmashauri ya Mji wa Mbinga	36	Utiri
		22	Halmashauri ya Wilaya ya Songea	37	Mpitimbi
10.	SONGWE	23	Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi	38	Ilolo
				39	Hasanga
				40	Ihanda
11	MTWARA	24	Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	41	Nanhyanga
				42	Namikupa
12	DODOMA	25	Halmashauri ya Jiji la Dodoma	43	Dodoma Makulu
13	MARA	26	Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti	44	Geitasamo
14	SIMIYU	27	Halmashauri ya Wilaya Bariadi	45	Nkundwabiye
		28	Halmashauri ya Mji wa Bariadi	46	Nyangokolwa